**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MPANGO WA SERIKALI YA AWAMU YA SITA WA KUWAENDELEZA WATUMISHI WA SEKTA YA AFYA KATIKA FANI ZA UBINGWA NA UBINGWA BOBEZI NCHINI *(SAMIA HEALTH SUPER SPECIALIZATION PROGRAM)*

**Dodoma, 28 Oktoba, 2022**

**Ndugu Wanahabari,**

Kama mnavyofahamu kuwa Serikali imekuwa ikifanya maboresho mbalimbali katika Sekta ya Afya. Maboresho hayo yanahusisha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, kutoa ajira mpya za watumishi wa afya katikam ngazi nzote, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa pamoja na kuwekeza kwenye maendeleo ya rasilimaliwatu ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya na zenye viwango vinavyokubalika. Pamoja na uwekezaji unaofanywa, nchi bado inakabiliwa na uhaba wa wataalamu bingwa (Specialists) na bobezi (Super Specialists) wa kutoa huduma za afya.

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinawatumishi wenye weledi na ujuzi wa hali ya juu, Wizara ya afya ilijiwekea lengo la miaka mitano (2020-2025) la kusomesha wataalamu bingwa na bobezi

wasiopungua **300** kwa kila mwaka wa fedha. Katika utekelezaji wa mpango huo kwa kipindi cha miaka miwili (2020/21 na 2021/22) Wizara imefanikiwa kusomesha wataalamu bingwa **524** ambao wanaendelea na masomo kwenye vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Lengo la mpango huu ni kuimarisha huduma za kibingwa na bobezi nchini ili kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopata rufaa za matibabu nje ya nchi.

Hadi kufikia Disemba 2021, mahitaji ya wataalamu bingwa katika Hospitali zinazotoa huduma za kibingwa na kibobezi nchini yalikuwa **1,782** wakati huo Serikali ilikuwa imeshawasomesha wataalamu **992** wa fani mbalimbali za kibingwa na kibobezi. Hatua hii imewezesha uboreshaji wa huduma za afya za kibingwa na bobezi katika hospitali mbalimbali nchini hali ambayo imechangia kuimarika kwa huduma za matibabu nchini na hivyo, idadi ya wagonjwa wanaopata rufaa ya matibabu nje ya nchi imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka. Mfano katika kipindi cha mwaka 2014/15 (wagonjwa 683), 2015/16 (wagonjwa 385), 2020/21 (wagonjwa 56) na hadi kufikia Machi 2021/22 jumla ya wagonjwa walikuwa 37.

Serikali kupitia Wizara ya Afya imefanya jitihada mbalimbali za kuboresha huduma za kibingwa na bobezi kwa kuongeza bajeti ya kuwaendeleza watumishi wa Sekta ya Afya. Kwa mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imeongeza fedha za kusomesha wataalamu bingwa na bobezi hadi kufikia shilingi **Bilioni 8** kutoka Shilingi **Bilioni 3** za mwaka wa fedha 2021/22.

**Ndugu Wanahabari,**
Ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na bobezi nchini kuanzia mwaka huu wa fedha, Wizara imeanzisha mkakati mpya wa kutoa ufadhili kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa utaratibu wa ***set.*** Kupitia utaratibu huu, utahusisha kusomesha timu za wataalamu wanaohitajika kwa ajili ya kukamilisha utoaji huduma za kibingwa na bobezi. Utaratibu huu umeanzishwa ili kuhakikisha huduma za kibingwa zinazotolewa zinakuwa na wataalamu wote wanaohitajika ili huduma husika iweze kutolewa kwa ukamilifu. Watumishi hao wanapochaguliwa kwenda kusoma wanakuwa kwenye *set* ya wataalamu wa fani mbalimbali watakaokamilisha huduma

husika mfano matibabu ya upandikizaji figo (Renal Transplant) na matibabu ya saratani (Oncology).

Mfano, wataalamu watakaosomeshwa kwa ajili ya kutoa huduma ya matibabu ya figo kikamilifu katika ***set*** ni kama ifuatavyo; Daktari Bingwa wa Upasuaji figo, Daktari Bingwa wa matibabu ya figo, Daktari Bingwa wa utoaji dawa ya Usingizi kwa wagonjwa wa figo, Daktari Bingwa wa Mionzi, Muuguzi Bingwa wa Mionzi, Mteknolojia Mionzi, Muuguzi Bingwa wa figo, Muuguzi Bingwa wa Usimamizi wa huduma za chumba cha upasuaji kwa wagonjwa wa figo na Mtaalamu wa Vifaa Tiba vinavyotumika kwa ajili ya matibabu ya figo.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia Mpango wa kufadhili watumishi wa Afya katika fani za ubingwa na ubobezi, Wizara itatoa ufadhili wa mafunzo ya *set* yaliyowasilishwa na Taasisi mbalimbali katika maeneo ya kibobezi na kibingwa kupitia mpango huu wa *set*, ambapo jumla ya watumishi **139** wamechaguliwa kupata ufadhili wa masomo ambapo kati ya hao **136** watasomeshwa nje ya nchi na **3** ndani ya nchi. Tunamshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kuongeza fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 8** zitakazotumika kugharamia wataalamu waliochaguliwa kusoma mafunzo haya kwa lengo la kuwa na wataalamu wa kutosha kukamilisha mahitaji ya utolewaji wa huduma katika fani husika za kibingwa na bobezi .Ili kumuenzi Mhe. Rais Samia kwa uamuzi wake huu mkubwa wa kuhakikisha ukamilifu wa huduma za kibingwa na bobezi Mpango huu umepewa jina la ***Mpango wa Samia wa kuongeza wataalamu bingwa na bobezi wa afya nchini (Samia Health Super Specialization Program in Tanzania).***

Hospitali zitakazonufaika kupitia na Mpango huu ni pamoja na;

**Hospitali ya Taifa Muhimbili**

i. Upandikizaji figo.
ii. Upandikizaji uroto (Bone Marrow Transplant).
iii. Upandikizaji wa vifaa vya kusikia (Cochlear Implant).
iv. Upasuaji bobezi wa kinywa na uso.

**Hospitali ya Mloganzila**

i. Ubobezi katika huduma za tiba za mfumo wa upumuaji.
ii. Ubobezi katika huduma za wagonjwa wa kiharusi.

**Hospitali ya Benjamin Mkapa**

i. Ubobezi katika huduma za figo.
ii. Ubobezi katika hduma za Saratani.
iii. Upandikizaji uroto.

**Taasisi ya Mifupa Muhimbili**

i. Upasuaji wa mishipa ya damu kwenye ubongo na uti wa mgongo.
ii. Mazoezi tiba katika maradhi yanayotokana na ajali.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC**

i. Matibabu ya kibobezi katika afya ya Ngozi.
ii. Huduma za Utengamao.
iii. Huduma za mfumo wa Mkojo.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando**

i. Huduma za kibingwa za matibabu ya Saratani.

**Taasisi ya Saratani ya Ocean Road**

ii. Ubobezi katika upasuaji wa Saratani.
iii. Ubobezi katika tiba mionzi tiba na nyuklia (Radiotherapy & Nuclear Medicine.

**Ndugu Wanahabari,**

Sambamba na kufadhili watumishi **139** kwa utaratibu wa *set* pia watumishi **318** watafadhiliwa kwa utaratibu wa mtu mmoja mmoja. Hivyo jumla ya watumishi watakaofadhiliwa ni **457** kwa mwaka wa fedha 2022/23, ambapo **146 (32%)** ni wanawake. Kati ya watumishi **457** watakaofadhiliwa, **157 (34%)** watasoma kwenye Taasisi za nje ya nchi.

Ufadhili huu, ni kwa ajili ya malipo ya ada kwa asilimia mia moja ya chuo husika na posho ya utafiti kwa waliopata ufadhili kwa vyuo vya ndani ya nchi. Kwa watakaofadhiliwa nje ya nchi watalipiwa ada kwa asilimia mia moja, posho ya utafiti, nauli pamoja na posho ya kujikimu wakiwa masomoni. Majina ya wote waliochaguliwa kupata ufadhili kwa mwaka 2022/23 kwa mchanganuo nilioutaja hapo juu yatapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Afya (www.moh.go.tz)

**Ndugu Wanahabari,**

Pamoja na ufadhili kwa watumishi **457**, jumla ya watumishi **524** wanaendelea na masomo katika fani mbalimbali za kibingwa na bobezi, hivyo kupelekea idadi ya wataalamu bingwa wanaofadhiliwa na Serikali kuwa **981**. Jitihada hizi za Serikali zitaongeza idadi ya wataalamu bingwa na bobezi wanaohitimu kila mwaka ikilinganishwa na watumishi **259** waliohitimu mafunzo hayo kwa mwaka 2021/22.

**Ndugu Wanahabari,**

Wizara inatambua kuwa zipo taaluma ambazo bado zinauhitaji mkubwa nchini lakini kuna mwamko mdogo wa watumishi kuomba kusoma fani hizo. Taaluma hizo ni pamoja na wataalamu wa kutoa dawa ya usingizi (Anaesthesiologist), wataalamu wa upasuaji ubongo na mishipa ya fahamu (Neurosurgeon), Wataalamu wa Tiba ya mishipa ya fahamu (Neurologist) Wataalamu wa Afya ya Akili (Psychiatry and Mental Health Specialist), Wataalamu wa Patholojia (Anatomical Pathologist), Wataalamu wa tiba ya

Saratani (Oncologist), Wataalamu wa tiba ya Damu (Haematologist), wataalamu wa upasuaji wa Pua, Masikio na Koo (ENT Surgeon) na wataalamu wa tiba ya Kinywa na Meno (Oral and Dental specialties). Serikali kupitia Wizara ya Afya, inapenda kuwahamasisha watumishi kuendelea kujitokeza kuomba ufadhili katika fani hizo.

**Ndugu Wanahabari,**
Napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha na kuwasisitiza watumishi wote wanaonufaika na ufadhili huu wa Serikali kupitia Wizara ya Afya, kukumbuka kuwa Serikali inafanya jitihada zote hizi ili kuboresha huduma za afya kwa ujumla wake, hivyo ni lazima waheshimu makubaliano ya kimkataba waliyoingia na Serikali pindi wanapohitimu ili kuboresha huduma kama ilivyokusudiwa. Wizara haitosita kuchukua hatua kali za Kisheria kwa wale wote ambao wamesomeshwa na kisha kukiuka masharti ya mkataba walioingia na Serikali.

Nichukue fursa hii pia kuwakumbusha Wakuu wa Hospitali na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Afya kuwa ni lazima watenge fedha kwenye bajeti zao kwa ajili ya kuwasomesha wataalamu bingwa kwa kila mwaka na taarifa ya idadi ya wale watakaosomeshwa iwasilishwe Wizarani. Utekelezaji wa mpango huu uanze rasmi kuanzia mwaka wa fedha ujao yaani 2023/2024.

Mwisho kabisa niendelee kumshukuru sana Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonyesha kwa vitendo jitihada zake za kutaka kufanya mapinduzi katika Sekta ya Afya. Tuna imani kubwa kuwa maboresho haya yataendelea na wananchi wataendelea kunufaika na huduma bora za Afya nchini.

Imetolewa na:

Ummy A. Mwalimu (Mb)
**WAZIRI WA AFYA**